# Hifadhi Kadi na PIN Yako kwa Usalama

## Kadi ya Huduma

- Hifadhi kadi yako sehemu salama, kama vile kwenye pochi au mkoba wako.
- Weka kadi yako katika hali ya usafi, mbali na mwanga wa moja kwa moja wa jua na mbali na sumaku na vifaa vya elektroniki.

## Usalama wa PIN

- Usishiiriki PIN yako na mtu yeyote.

## Kubadilisha Kadi/PIN

- Ikiwa utasahau PIN, piga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC kwenye namba **1-844-230-0813** au ingia kwenye **www.ebtEDGE.com** au kwenye **programu ya FIS ebtEDGE** ili kuibadilisha.
- Ikiwa kadi yako imepotea, kuibiwa au kuharibika, piga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC kwenye namba **1-844-230-0813**. Kadi zitabadilishwa kupitia barua ya kawaida. Unapaswa kupokea kadi yako ndani ya siku tano hadi saba.
- Au, tembelea kliniki ya WIC ya eneo lako ili kubadilisha kadi yako.

## Itakuwaje nikisahau PIN yangu au nikikosea wakati wa kuingiza?

Ukiingiza PIN yako na kukosea mara 4 mfululizo, kadi yako itafungwa hadi saa sita usiku. Unaweza kubadilisha PIN yako kwa kupiga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC au kwa kuingia kwenye **www.ebtEDGEcom** au kwenye programu ya FIS **ebtEDGE**. Usipoweka upya PIN yako, kadi yako itafunguliwa kiotomatiki saa sita usiku, hata hivyo, bado utatakiwa kujua PIN yako ili uweze kutumia kadi yako.

# Ifikie kwa Urahisi

**Tembelea www.ebtEDGE.com, pakua programu ya FIS ebtEDGE, au piga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC.**

Ili kuangalia salio la manufaa, historia ya manunuzi na taarifa za akaunti:

Piga simu ya **Huduma kwa Wateja ya eWIC** bila malipo inayopatikana 24/7 kwa:

**1-844-230-0813**

**AU Tembelea**

**www.ebtEDGE.com**

**AU**

**Tumia programu ya FIS ebtEDGE**

Tumia programu ya **FIS ebtEDGE au www.ebtEDGE.com** ili:

- Kuangalia manufaa ya chakula ya sasa
- Kuweka, kubadilisha au kufungua PIN yako
- Kutazama historia ya miamala
- Kutazama manufaa yajayo
- Kuagiza kadi mpya
- Kurejesha nenosiri au jina la mtumiaji
- Kutazama mahali duka lilipo

**Maswali?** Wasiliana na kliniki ya WIC katika eneo lako au tembelea tovuti kwa www.ncdhhs.gov/ncwic/eWIC

Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya NC, Kitengo cha Ustawi wa Mtoto na Familia, Sehemu ya Huduma za Lishe kwa Jamii • www.ncdhhs.gov/nc-wic-cacfp
Taasisi hii inatoa fursa sawa kwa wote.

THE GREAT SEAL OF THE STATE OF NORTH CAROLINA
MAY 20, 1775 APRIL 12, 1776
ESSE QUAM VIDERI

#0016
24419I100

# Kutumia Kadi yako ya eWIC ya North Carolina




## Rahisi, Salama na Inafaa

# Kuanza: Chagua PIN

Kabla ya kutumia Kadi yako ya eWIC ya North Carolina, lazima uchague Nambari ya Utambulisho Binafsi (PIN) yenye tarakimu 4.

## Piga simu, ingia mtandaoni au pakua programu

- Piga simu kwenye Huduma kwa Wateja ya eWIC kwa **1-844-230-0813**
- Iingia kwenye **www.ebtEDGE.com**
- Au, tembelea duka lako la programu ili upakua **programu ya FIS ebtEDGE**

## Chagua PIN

- Lazima uchague Nambari ya Utambulisho Binafsi (PIN) yenye tarakimu 4 kwa ajili ya kadi yako.
- Chagua nambari ya tarakimu 4 ambayo ni rahisi kwako kuikumbuka lakini ni ngumu kwa wengine kubashiri.
- Usiandike PIN yako kwenye kadi yako au kwenye kitu chochote unachohifadhi pamoja na kadi yako.

Ni lazima uwe
na Kadi yako ya eWI
ya North Carolin
unapokuwa dukani ili uweze
kutumia manufaa yako ya
WIC.




# Kutumia kadi yako

Unaweza kutumia kadi yako mahali popote ambapo eWIC ya North Carolina inapokelewa.

## Fanya Manunuzi ya Vyakula vya WIC

- Kuwa na taarifa ya salio la manufaa yako ya chakula ya WIC unapokwenda dukani.
- Tumia Orodha ya Vyakula Vilivyoruhusiwa na WIC kukagua ni vyakula gani vinavyoruhusiwa.

## Kamilisha manunuzi yako

- Inawezekana ukahitaji kutenganisha vyakula vya WIC mbali na vyakula visivyo vya WIC.
- Ingiza PIN yako yenye tarakimu 4 ukiombwa kufanya hivyo.
- Hifadhi stakabadhi yako - inaonyesha salio la manufaa yako.

## Fuata sheria za Mpanngo wa WIC

- Unaweza kuondolewa kwenye Mpango wa WIC ikiwa utatumia vibaya kadi au manufaa yako.
- Usiuze kadi yako ya eWIC, vyakula vya WIC, au maziwa ya WIC ya watoto.
- Kununua, kuuza au vinginevyo kutumia vibaya manufaa ya WIC ni kosa kisheria. Kutoa taarifa kuhusu udanganyifu unaoshukiwa, piga simu kwa 800-424-9121 au tembelea www.usda.gov/oig/hotline.htm.
- Usirejeshe vyakula vya WIC au maziwa ya watoto ili upewe fedha au mkopo.

## Usalama wa Kadi

Ikiwa mtu atapata kadi yako na kujua PIN yako, anaweza kutumia manufaa yako. Manufaa hayo hayatafidiwa Kwa vidokezo zaidi vya usalama, tazama nyuma ya kipeperushi chako.

# Kuelewa Manufaa Yako

Ni muhimu kujua unapopokea manufaa yako.

## Upatikanaji wa Manufaa

- Manufaa yako huanza kupatikana katika **Tarehe ya Kuanza kwa Manufaa** saa 6 kamili usiku na kuisha saa 5 na dakika 59 usiku katika **Tarehe ya Kuisha kwa Manufaa.**
- Manufaa ambayo **hayakutumiwa HAYAJUMUISHWI** kwenye kipindi cha manufaa kinachofuata.

## Tazama salio lako la manufaa

Ili kukagua salio lako fanya mojawapo kati ya haya yafuatayo:

- Tazama risiti yako ya mwisho.
- Ingia kwenye **www.ebtEDGE.com**.
- Angalia kwenye programu ya **FIS ebtEDGE**
- Piga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC kwenye **1-844-230-0813**.

## Mahali pa kupata msaada

- Kwa maswali kuhusu kadi yako ya eWIC ya North Carolina, tafadhali ingia kwenye www.ebtEDGE.com, programu ya FIS ebtEDGE au piga simu kwa Huduma kwa Wateja ya eWIC kwenye 1-844-230-0813.
- Kwa maswali kuhusu manufaa yako ya chakula ya WIC, au ikiwa utahamia au kubadilisha anwani yako, tafadhali wasiliana na kliniki yako ya WIC ya karibu.
- Kwa taarifa za jumla kuhusu mpango wa WIC wa North Carolina, wasiliana na kliniki yako ya WIC katika eneo lako au tembelea tovuti yetu kwenye www.ncdhhs.gov/ncwic/eWIC.